

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA



Juni 15, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili Dhidi ya Wazee Juni 15, 2023

Tarehe 15 Juni ya kila mwaka ni Siku ya Kimataifa ya kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya wazee. Lengo la siku hii ni kuikumbusha jamii umuhimu wa kuwaenzi na kuwasikiliza wazee kuhusu hali zao sambamba na kuacha vitendo vya ukatili, manyanyaso na udhalilishaji dhidi ya wazee. Kauli Mbiu ya maadhimisho ya mwaka 2023 ni: "**Wazee Wanastahili Heshima na Usikivu Wetu.**"

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ikiwa ni chombo chenye mamlaka kitaifa katika kulinda, kukuza na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora, inaungana na wadau wote nchini katika maadhimisho hayo.

THBUB inatambua, kuthamini na kupongeza jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kushughulikia masuala mbalimbali yanayowakabili wazee, ikiwa ni pamoja na:

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Ploti Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/Ploti Na. 201, Mtaa wa Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: info@chrapp.go.tz, zanzibar@chrapp.go.tz; Tovuti: www.chrapp.go.tz

- i) Kutoa vitambulisho vya matibabu bure (ICHF) kwa wazee wasiojiweza;
- ii) Kuanzishwa kwa Baraza la Wazee katika ngazi ya kitaifa na mabaraza ya wazee katika ngazi mbalimbali kote nchini;
- iii) Kutenga vyumba na watumishi maalum kwa ajili ya wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya;
- iv) Kuanzisha Dawati la kuratibu huduma za afya kwa Wazee katika ngazi ya Wizara na katika Halmashauri;
- v) Kuweka madirisha ya wazee katika hospitali na vituo vya afya;
- vi) Kuanzisha mchakato wa malipo ya pensheni kwa wazee wote;
- vii) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kulipa Pesheni Jamii kwa wazee wote wenye umri wa miaka 70+; na
- viii) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuendelea kuhudumia wastaaifu.

Pamoja na jitihada hizo, wazee bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kuuliwa, kunyanyaswa na kupigwa kutokana na imani za kishirikina.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa upande wake imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha kuwa haki za wazee zinalindwa na kuhifadhiwa ikiwemo kupokea na kuyashughulikia malalamiko ya wazee na kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na haki za wazee.

Kupitia siku hii, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inapendekeza yafuatayo:

- i) Serikali iharakishe mchakato wa kutunga sheria maalum ya Wazee ili haki za wazee zilindwe kisheria;
- ii) Serikali ishirikiane na wadau mbalimbali kutoa elimu kwa jamii kuachana na ukatili dhidi ya wazee; na
- iii) Watanzania wote kuendelea kupinga vitendo vyote vyta ukatili dhidi ya wazee.

Mwisho, Tume inatoa wito kwa wananchi wote kwa pamoja tutekeleze wajibu wetu kwa wazee kwa kuhakikisha tunawalea, tunawaheshimu, tunawapatia ulinzi, usalama, chakula, mavazi na malazi.

“Tuhakikishe wazee wanalindwa, wanasikilizwa, kupewa heshima na usikivu wa kila Mtanzania.”

Imetolewa na:



Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)
Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Juni 15, 2023